# TASAFIC

*Elimu na Umoja Tuijenge Tanzania*

*TASAFIC inakaribisha matangazo mbali mbali ya kibiashara katika majarida yajayo. Wasiliana moja kwa moja na TASAFIC*

Toleo 0002

Agosti 2024

Ukurasa 1

Tanzania Students Associations Federation in China| c/o. Tanzania Embassy in Beijing 8 LiangMa He Nan Lu, Sanlitun, 100600 Beijing, P.R. CHINA| TASAFICtc@gmail.com

*Kwa habari zaidi www.TASAFIC.com*


## Habari

### Kurugenzi ya Uchumi na Fedha TASAFIC 2024/2025 wafanya kikao cha kwanza

Kutoka TASAFIC

Mnamo wa mwezi wa nane Kamati ya Uchumi na Fedha ilikutana kujadili masuala ya mpango wa fedha kwa mwaka 2024/2025.

Katika kikao hicho ambacho wajumbe wake ni Wahazina wa jumuiya ambazo ni wanachama wa TASAFIC. Walijadiliana kwa pamoja kuhusu ukusanyaji wa vyanzo vya mapato TASAFIC. Kwa sasa mapato yaliyopo ni ada za Jumuiya wanachama na mavazi ya kuitangaza Tanzania kama Fulana, Kofia, Vikoi, na Viatu vya wazi.

Katika kikao hicho wajumbe walitakiwa kutangaza bidhaa hizo ili kuweza kuwafikia wanachuo wengi wa Kitanzania waliopo China.

Pia kamati inakaribisha mawazo ya kibiashara ambayo wanajumuiya wanayo ili yaweze kutumika kwa ajili ya kuiendeleza TASAFIC.

## Yaliyomo ndani


**Makala ya Elimu……………………..Uk 2**

**Makala ya Biashara…….…..………..Uk 2**

**Matangazo…….…..…………………..Uk 2**


## Habari katika picha



## TASAFIC Pichani

***Pichani:*** *Viongozi wapya wateule wa 2024/2025 wa TASAFIC waliochaguliwa na Jumuiya za wanafunzi wasomao nchini China kupitia uwakilishi wa viongozi wao walipokutana katika kikao chao cha kwanza nchini China. Kutoka kulia ni Naibu Katibu Mkuu-Paschal Jao, Makamu Mwenyekiti-Janeth Nyandiwa Mnyaga, Mwenyekiti-Sabatho Jivitius Ching'oro, Katibu Mkuu-Chitalika Elieza, na Mweka Hazina -Juliana Kauno .*

## Waandaaji wa Jarida


**Mhariri Mkuu- Martin Faustin Itangaja**

**Mpangilio na Uandishi– Paschal Jao**

**Picha- Janeth Nyandiwa Mnyaga**

**Matangazo- Juliana Kauno**


## Ujumbe wa wanafunzi wa mwaka wa masomo 2024/2025Kutoka katika Jumuiya za TASAFIC nchini China

### RUKAIYA ALI ABDULRAHMAN– Harbin Institute of Technology

Niliwasili China mwishoni wa mwezi wa nane 2024, safari ilikuwa ndefu kutokana na mabadiliko ya usafiri. Lakini namshukuru Mungu nilifika salama na kupokelewa vizuri na wenyeji wangu ambao ni Watanzania wanaosoma nchini China.

Nimechaguliwa kuja kusoma chuo kinaitwa Harbin hapa China. Kwa sasa tunaendelea na usajili, pamoja na kuzoea mazingira ya China, kwa kuwa ndiyo sehemu tutakayokaa muda mrefu hadi tutakapohitimu masomo yetu na kurudi Tanzania kuitumikia nchi yetu kwa yale tuliyojifunza nchini China.

Ninawashauri Watanzania wenzangu kuchangamkia fursa za kielimu nchini China sababu zipo nyingi sana ukilinganisha na nchi zingine duniani kote.

### SHARON E. MUNISI -Zheijiang Normal University

Ninafuraha kubwa kupata nafasi hii katika jarida la TASAFIC, Natanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mh. Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na Mh. Balozi Khamis Mussa Omar kwa juhudi zao katika kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na China. Maneno pekee hayawezi kutosha kufikisha Shukrani hizi mbele yenu.

Mwaka 2023 nilipata nafasi ya kuja China na kushuhudia fainali mashindano ya lugha ya Kichina kwa vyuo vikuu, nilistaajabishwa na jinsi dunia inavyoijua Tanzania, na hii ni kwa sababu ya juhudi za mama yetu Mh. Rais Samia alizoweka katika kutengeneza filamu ya "Royal Tour". Hivyo nilijivunia sana kuwa Mtanzania.

Sasa ni 2024 nimepata nafasi ya masomo nchini China. Nimefurahi sana kwa kupata nafasi hii ya bahati. Mwishoni ningependa kuhamasisha Watanzania kufika kwa wingi nchini China kwa fursa za Masomo, Biashara, na Ajira .

### Daniel Christopher Peterson- Graduate School of Chinese Academy of Agricultural Sciences

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na afya njema, pia nashukuru na kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendeleza mahusiano mazuri ya kidiplomasia na nchi ya Jamhuri ya Watu wa China. Matokeo ya mahusiano ya nchi hizi mbili yamepelekea China na Tanzania kuendelea kushirikiana katika nyanja mbalimbali zikiwemo za Kiuchumi, Kisasia, Kijamii, Kitamuduni, Kielimu n.k.

Nilifanikiwa kupata ufadhili wa masomo wa Serikali ya China kusoma shahada ya Uzamili 2019/21. Pia 2024 kusoma Shahada ya Uzamivu. Ninawashauri Watanzania kuchangamkia fursa mbalimbali zinazopatikana na kutolewa na nchi ya China hasa fursa za ufadhili wa kimasomo, pia hata fursa zingine kama vile za kibiashara.

Nawashauri Watanzania kuwa wazalendo, waadilifu, wachapakazi, kuwa na tabia njema, kutenda haki, na kudumisha amani ya Taifa letu la Tanzania .

## Ujumbe kutoka kwa Mwenyekiti– Sabatho Jivitius

Habari za likizo Watanzania wote mliopo China na wengine ambao mlirudi likizo nyumbani nchini Tanzania.

Napenda kuwatakia maandalizi mema ya kuanza mwaka mwingine wa masomo 2024/2025 hapa nchini China. Pia niwatakie safari njema wote ambao mtakuwa njiani kurejea nchini China.

Jambo la muhimu kuzingatia siku zote ni kufuata sheria za nchi ambayo tupo bila kuzivunja, pia tuzingatie masomo na sheria za vyuo husika tunavyosoma.

Viongozi wa Jumuiya husika tuendelee kupokea wanafunzi wapya ambao wamechaguliwa kuja kuungana nasi katika safari hii ya kimasomo hapa nchini China.

Asanteni sana wote, na niwatakie mwaka mpya wa kimasomo.

TASAFIC "ELIMU NA UMOJA, TUIJENGE TANZANIA"










ELIMU

ELIMU

ELIMU

ELIMU

## Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Lugha za Kigeni cha Tianjin (Tianjin Foreign Studies University)

*Na Martin Faustin Itangaja.*– Tianjin

Chuo Kikuu cha Lugha za Kigeni cha Tianjin (Tianjin Foreign Studies University) ni chuo maarufu kimojawapo kinachobobea ufundishaji wa lugha za kigeni nchini China. Na Idara yake ya Kiswahili ilianzishwa rasmi mwaka 2006, mwaka 2007 ikaanza kuwaandikisha wanafunzi kila baada ya mwaka mmoja. Kuanzia mwaka 2016 ikaanza kuwaandikisha wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiswahili kufanya utafiti kuhusu Afrika. Mwaka 2020 idara yenyewe ilitunukiwa kozi maalum ya kimkoa, na mwaka 2021 ikatunukiwa kozi maalum ya kitaifa ambayo ni sifa ya kipekee iliyopatiwa na vyuo viwili tu nchini China mpaka sasa. Idara yetu ya Kiswahili imechangia sana maendeleo ya Kiswahili nchini China. Katika idara hiyo, kwa jumla kuna walimu watano, mmoja ni Mtanzania anayeitwa Martin Faustin Itangaja. Na mkuu wa sasa anaitwa Zhouli aliyewahi kupata umahiri wa Kiswahili UDSM na baruapepe yake ni 869997842@qq.com.

**1. Malengo ya Mafunzo na Matarajio ya Kazi**

***- Malengo ya Mafunzo:***

Kozi hii inalenga kukuza wanafunzi wenye upendo kwa nchi, wana mtazamo wa kimataifa, wanaofuata kanuni za kimataifa, na wana heshima ya maarifa ya kibinadamu. Wanafunzi wanatakiwa kuwa na uelewa wa kina wa lugha ya Kiswahili, maarifa ya fasihi na utamaduni wa Kiswahili, na kuwa na uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili. Wanafunzi watajengewa uwezo wa mawasiliano ya kimataifa, utamaduni, na kushiriki katika mambo ya kimataifa. Pia wataweza kushiriki katika shughuli za elimu, tafsiri, ukalimani na kazi nyingine zinazohusiana na lugha ya Kiswahili. Mwishowe, wanatarajiwa kuwa wataalamu wenye ujuzi wa kina na uwezo wa kufanya kazi katika mazingira ya kimataifa.

***- Matarajio ya Kazi:***

Kiswahili ni moja ya lugha kuu tatu za Kiafrika, na ni lugha rasmi katika nchi kadhaa za Afrika. Kwa sababu ya kuanzishwa kwa “Ukanda na Barabara” (Belt and Road Initiative) na ushirikiano kati ya China na nchi za Afrika, hasa nchi za Afrika Mashariki, kuna mahitaji makubwa ya wataalamu wa lugha ya Kiswahili. Wahitimu wa kozi hii wanaweza kufanya kazi katika nyanja mbalimbali kama vile biashara za kimataifa, diplomasia, elimu, utamaduni, na utalii, wakichangia katika ushirikiano kati ya China na Afrika.

**2. Sifa za Mafunzo**

Chuo Kikuu cha Lugha za Kigeni cha Tianjin kilianzisha kozi ya Kiswahili kama sehemu ya mpango wa kitaifa wa kuongeza maarifa ya lugha za Kiafrika. Idara hii imepitia awamu kadhaa za maendeleo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2006, na sasa imekuwa kituo kikuu cha kufundisha Kiswahili nchini China. Wahitimu wanajengewa uwezo wa vitendo katika mazungumzo ya Kiswahili, pamoja na maarifa ya kina ku- husu utamaduni wa Kiswahili. Shule pia inasisitiza umuhimu wa ushirikiano wa timu, ubunifu, na maadili ya kitaaluma.

**3. Mafunzo ya Kawaida**

Chuo hiki kinatoa kozi mbalimbali kuanzia ngazi ya chini (shahada ya kwanza) hadi ya juu (shahada ya pili) katika lugha ya Kiswahili. Kozi hizi ni pamoja na sarufi ya Kiswahili, fasihi ya Kiswahili, tafsiri na ukalimani, pamoja na mafunzo ya kuandika na kusoma katika Kiswahili. Wahadhiri ni wataalamu wa lugha ya Kiswahili na wana uzoefu mkubwa katika kufundisha lugha hii.

**4. Mazingira ya Kazi ya Vitendo**

Wanafunzi wa Kiswahili wanapata nafasi za kufanya mafunzo ya vitendo katika Taasisi za Ushirikiano kati ya China na Afrika. Shule inawashauri wanafunzi kushiriki katika programu za mafunzo ya kimataifa na kufanya mazoezi nje ya nchi. Shule pia inawasaidia wanafunzi kupata uzoefu wa kufanya kazi na mashirika ya kimataifa na kujifunza mambo mbalimbali yanayohusu lugha ya Kiswahili katika mazingira halisi.

**5. Nafasi za Wahitimu**

Wahitimu wa kozi ya Kiswahili wana uwezo wa kuingia katika sekta mbalimbali kama vile tafsiri, elimu, biashara ya kimataifa, utamaduni, na utalii. Wanaweza kupata kazi katika makampuni ya kimataifa, ofisi za ubalozi, vyuo vikuu, na taasisi za utafiti. Wahitimu wa shule hii wana kiwango cha juu cha ajira, na wengi wao wanapata nafasi nzuri za kazi nchini China na Afrika.


**MATANGAZO HAPA WASILIANA NA TASAFIC**



**MATANGAZO HAPA WASILIANA NA TASAFIC**


Biashara

Biashara

Biashara

## Mambo muhimu ya kuzingatia unapoanzisha Biashara

*J.A , Paschal – Sichuan . IG na X: Pj_jaofficial*

Karibuni wote katika mtiririko huu wa Makala za biashara ambazo nitakuwa nikizielezea kila wiki. Leo katika Makala hii nitaelezea umuhimu wa kuyafahamu mambo muhimu pale unapopanga kuanza biashara kwa mtu ambaye ndio unaanza kabisa biashara. Tutajifunza kulingana na eneo husika hasa Tanzania na nchi za Afrika mashariki, kwa maana biashara yoyote ile duniani inatofautiana kutokana na maeneo, ukanda, nchi zilizoendelea na zinazoendelea.

**1. Utafiti wa Soko**

Watu wengi kabla ya kuanza biashara wanayoitaka wamekuwa hawafanyi utafiti wa kulielewa soko la biashara wanayotaka kuianza, wengine wanaangalia au kwa kusikia au kwa kuona mtu fulani katika biashara anauza sana na anapata wateja sana bila kufahamu kinachoendelea. Kufanya utafiti wa soko kabla ya biashara itakusaidia kubaini wateja wako watarajiwa, mahitaji yao, mapendeleo yao, na tabia zao. Hili litakusaidia kurekebisha mpangilio wa bidhaa au huduma utakazoziuza kwa wateja wako, pia kuweka vyema biashara yako dhidi ya washindani wako.

**2. Mpango wa Biashara**

Kumbuka kwamba biashara iliyopangiliwa na kuundwa vizuri ni kama ramani ya mafanikio yako kibiashara, kama mfanyabiashara ni lazima kuelewa malengo yako katika biashara unayotaka kuianza, soko lililodhamiria, thamani ya biashara yako, mtiririko wa mapato,mikakati ya uuzaji katika biashara hiyo. Kumb Kumbuka kuwa na mpango mzuri wa kibiashara unaweza kuvutia wawekezaji au wafadhili katika biashara unayopanga kuianza.

**3. Usimamizi wa Fedha ni Muhimu**

Usimamizi wa fedha kwenye biashara yoyote ile inayoanza na kuendelea ni muhimu sana. Unahitaji kuelewa vizuri gharama zako za kuanzisha biashara ili kupata mtaji wa kutosha, kudhibiti mtiririko wa pesa kwa ufanisi, na kufuatilia gharama ili kuepuka mitego ya kifedha inayoweza kuua biashara yako

**4. Muundo wa biashara yako na masuala ya kuzingatia Sheria**

Ili kuleta matokeo mazuri ikiwemo uaminifu wako kwa wateja na kutii kanuni za kodi,leseni katika nchi yako.


**MATANGAZO HAPA WASILIANA NA TASAFIC**





Hii itasaidia zaidi wakati wa biashara wateja wako kupata uaminifu,uwazi jinsi unavyofanya biashara pamoja nao. Mara nyingi katika nchi zinazoendelea uaminifu na uwazi huwa ni mgumu sana hivyo hupelekea wanaoanza biashara kuiona ni ngumu sababu wale waliotangulia katika biashara waliwatapeli wateja wao.

**5. Uvumilivu kulingana na mabadiliko yanayojitokeza**

Zingatia hili mazingira ya biashara huweza kubadilika kila mara, hivyo kama mjasiriamali au mfanyabiashara kubali kubadilika kutokana na mazingira ya wakati huo. Na kujitayarisha kwa changamoto na vikwazo mbalimbali katika biashara. Muhimu zaidi ni ustahimilivu ambao utakusaidia sana katika kuja kushinda vizuizi na na kuendelea kukuza biashara yako kwa muda mrefu ambayo uliyoianzisha.

TANGAZO

### *Juliana Kauno- Mweka hazina wa TASAFIC*

***Kupitia jarida hili tunakaribisha wale wote wenye matangazo ya kibiashara na wale wenye utaratibu wa kutumiana fedha za kitanzania na fedha za kichina, basi wasiliana nasi kama TASAFIC kwa kupewa utaratibu mzuri.***

***Tutumie fursa hii ya Kielimu na kibiashara na zingine nyingi kupitia Jarida hili ambalo ni faida kwetu sote.***

***Unaweza pia kuwasiliana na Viongozi wa TASAFIC kwa matangazo.***

***KARIBUNI***

Uchaguzi Diaspora Guangzhou

### Mkurugenzi wa Elimu Diaspora Ghuangzhou 2024

*Dr Chiku Badru Mwimbo — Guangdong*

Dr.Chiku Badru Mwimbo ni daktari bingwa wa magonjwa ya dharura yaani “Emergency Medicine Specialist.” Kwa sasa yupo katika jimbo la Guangdong mji wa Guangzhou katika chuo cha Southern Medical anachukua shahada ya uzamivu yaani ‘PhD in Emergency Medicine’. Mnamo tarehe 4 mwezi wa nane 2024 ulifanyika uchaguzi wa viongozi wa jumuiya ya Wanadiaspora wa Kitanzania wanaoishi Guangdong kwa kifupi DITAG ambapo aligombea nafasi ya Mkurugenzi wa elimu na kufanikiwa kuchaguliwa kuhudumu nafasi hiyo. DITAG inasimamiwa na mlezi wetu ambaye ni Konseli Mkuu wa Konseli ya Guangzhou Mh.Khatibu Makenga.

Majukumu ya mkurugenzi wa Elimu DITAG ni pamoja na kuwaunganisha wanafunzi na jumuiya hiyo ili kuweza kunufaika na fursa mbalimbali zinazopatikana katika jumuiya hiyo, kutafuta na kuwaelimisha Watanzania juu ya fursa za ufadhili wa masomo pamoja na kuandaa midahalo mbalimbali ya kielimu kwa vijana wa Kitanzania.

“DITAG ni sehemu ndogo tu ya Watanzania wote wanaoishi China ingawa inabeba sehemu kubwa ya wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao nchini China. Kwa kuwa kuna shirikisho la wanafunzi wa Kitanzania wanaosoma nchini China ( TASAFIC) nikiwa kama mkurugenzi wa elimu DITAG nimedhamiria kufanya kazi bega kwa bega na shirikisho la wanafunzi TASAFIC ili yale mazuri tuliyodhamiria kuyafanya yaweze kunufaisha Watanzania wengi zaidi” alisema Dr. Chiku Badru Mwimbo .

Tanzania Students Associations Federation in China| c/o. Tanzania Embassy in Beijing 8 LiangMa He Nan Lu, Sanlitun, 100600 Beijing, P.R. CHINA| **tasafictc@gmail.com**

